## Tuzo

Tuzo ja kwanza ni euro elfu mbili. Tuzo ja pili ni euro elfu moja na tuzo ja tatu ni euro mia tano.

## Namna ya kuomba

Maombi yatatumwa UEM. Mwisho wa kutuma maombi itakuwa tarehe 30 Juni 2018.

## Kwa Mawasiliano


Uli Baege (Idara ya Afrika)
United Evangelical Mission
Rudolfstrasse 137
D-42285 Wuppertal

✆ +49 (0) 202 890 04-181
✉ africa@vemission.org

Kristina Neubauer (Idara ya Asia)
United Evangelical Mission
Rudolfstrasse 137
D-42285 Wuppertal

✆ +49 (0) 202 890 04-164
✉ asia@vemission.org





United Evangelical Mission
Communion of Churches on three Continents
Rudolfstrasse 137
D-42285 Wuppertal
✆ +49 (0)202 890 04-0
🖷 +49 (0)202 890 04-179
✉ info@vemission.org
www.vemission.org


Deutsches Zentralinstitut für soziale Fragen (DZI)
DZI Spenden-Siegel
Zeichen für Vertrauen


**Waliohusika**
Mchapishaji: United Evangelical Mission (UEM)
Mhariri: Brunhild von Local
Michoro: Britta Kläffgen
Picha: Robert Mugabe / UEM, Heinrich de Arienzo / UEM
Layout: MediaCompany GmbH · toleo hili: Aprili 2017


VEM

# Tuzo ja Undugu UEM 2018









## Maelezo kuhusu Tuzo

Mwaka 2018, kwa mara nyingine tena, Chama cha Missioni cha UEM, kitatoa tuzo ya udugu kwa mradi bora wa udugu Afrika, Asia na Ujerumani. Uamuzi huu ulifanyika katika Mkutano Mkuu wa UEM wa mwaka. Mradi utakaoanzishwa na wanawake kwaajili ya wanawake utapewa kipaombele; itaonyesha wazi walengwa watakavyoshirikishwa tangu kuanza kwa mradi. Miradi itakayoonekana kuwa bora zaidi itawasilishwa katika Mkutano Mkuu wa mwaka 2018 na kupewa tuzo za kitita cha pesa kati ya Euro mia tano hadi elfu mbili.

## Masharti ya kuchaguliwa

Vikundi vyote vya undugu katika UEM vinaweza kuomba kushiriki tuzo la undugu.

## Jopo la kutoa tuzo

Kamati ya undugu ya UEM itaamua ni miradi ipi itapata tuzo la undugu.

## Vigezo vya mradi

1. Mradi unatakiwa uwe ni ule uliobuniwa na wanawake na wenye lengo la kuwaendeleza wanawake.

2. Mradi uonyeshe jinsi walengwa watakavyo shirikishwa tangu kuanza kwa mradi.

3. Aina ya mradi haifungwi: inaweza kuwa kampeni, mradi wa ubunifu, au hata mradi wa kawaida wa undugu katika masuala ya maendeleo.

4. Mradi uzingatie vigezo vya UEM kuhusu miradi yaani:

**Uamuzi wa wanaundugu**
Maombi ya tuzo kwa UEM, sharti yawe ni uwamuzi wa pamoja wa washiriki wote wa mradi husika wa undugu.

**Mpango, ufuatiliaji na tathmini ya pamoja**
Mradi utatekelezwa kwa kuzingatia mpango, ufuatiliaji na tathmini ya pamoja (Planning, Monitoring, Evaluation, PME).

**Uandaaji wa mradi utakuwa katika maeneo mbalimbali.**
Uandaaji mradi angalau uzingatie maeneo mawili kati ya maeneo matano ya kazi za UEM:
Uchechemuzi/msaada wa kisheria
Diakonia
Maendeleo
Uinjilisti
Undugu

Mradi unaweza kutekelezwa na washiriki wa pande zote mbili au washiriki wote wa kanda pale inapowezekana.

**Elimu katika Utekelezaji**
Makanisa, vikundi na taasisi kutoka nchi zinazoshiriki watapaswa kuwawezesha watu wao kupitia semina, mikutano, makongamano na kazi zingine.

**Kutangaza mradi kwa kufikia watu wengi**
Makanisa au vyombo vya habari visivyo vya kidini vitaripoti kuhusu matukio, semina na kazi zingine za mradi unapokuwa unaendelea.